



TARI HABARI

Toleo No. 05

| Julai 2026

| www.tari.go.tz

7 Sabasaba
2026



TARI YAIBUKA MSHINDI WA TATU MAONESHU YA SABASABA 2026



Mkuu wa
Wilaya ya Kilwa
atembelea
banda la TARI
Sabasaba



Teknolojia za
TARI zang'ara
katika uhifadhi
wa mazingira
Sabasaba



TARI Yaendelea
Kuelimisha
Wadau kuhusu
Teknolojia za
Kilimo



BODI YA UHARIRI

MWENYEKITI

DKT. THOMAS BWANA
Mkurugenzi Mkuu TARI

KATIBU

DKT. SOPHIA KASHENGE
Mkurugenzi wa Uhaulishaji
Teknolojia, Biashara na
Mahusiano

WAJUMBE

EVELYNE MPASHA
Kaimu Meneja Menejimenti
ya Maarifa na Mawasiliano DKT.

RAJAB KANGILE
Kaimu Meneja wa uhaulishaji wa
teknolojia, uendeshaji wa
biashara na ushirikiano

DKT. ABDULLAH MKIGA
Kaimu Meneja wa Kituo,
TARI Kifyulilo

DKT. ANDEKILILE MWAMAHONJE
Mtafiti Mwandamizi

DEODATUS KIRIBA
Mtafiti Mwandamizi

WAANDISHI

MUGINI SINGIRA
Afisa Uhusiano kwa Umma

GERALD USIRI
Afisa Uhusiano kwa Umma

MARIA PAUL
Afisa Uhusiano kwa Umma

HOSEA R. BILATANGUYE
Afisa Uhusiano kwa Umma



NDUGU msomaji mpendwa,
karibu tena katika toleo letu la nne la
Jarida la TARI Habari.

TARI ina jukumu la kufanya utafiti,
kusimamia, kuratibu na kuhamasisha
matumizi ya teknolojia za kilimo nchini
ili kutatua changamoto za wakulima,
kuongeza tija na kuchangia maendeleo
endelevu ya sekta ya kilimo na taifa kwa
ujumla.

TARI katika mwaka wa fedha 2025/2026
ulioishia Juni, 2026 ilikadiriwa kukusanya
shilingi bilioni 124 kutoka katika vyanzo
vyake vya mapato na ilipanga kuendelea
na utafiti wa mbegu aina 56 za mazao
ya kimkakati, pamoja na kuboresha
teknolojia za afya ya udongo na matumizi
sahihi ya mbolea kwa zao la tumbaku ya
mvuke.

Aidha, taasisi ililenga kufanya tafiti
za magonjwa ya mazao, ikiwemo
fungashada (BBTV) kwenye migomba,
blaiti ya mikoroshu, pamoja na ubwiri
unga na mnyauko fusari katika zao la
koroshu. Sambamba na hilo, TARI ilipanga
kutafti teknolojia saba (7) za kuongeza
thamani ya mazao ya kilimo, kusafisha
na kuhifadhi aina 360 za mbegu za asili,
pamoja na kukusanya vinasaba 12,968.

Vilevile, TARI ilikusudia kuendeleza
kituo cha TARI Ifakara kuwa kituo mahiri
cha utafiti wa zao la kakao na kuendelea
na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya
za ngano katika mikoa ya Morogoro na
Tanga.

Mpendwa msomaji, ili kulinda maeneo
ya utafiti dhidi ya uvamizi, TARI ilipanga
kuendelea na ujenzi wa uzio katika
mashamba 10 ya utafiti; kulipa fidia kwa
wananchi watakaohamishwa katika kituo
cha TARI Uyole; kuhakikisha upatikanaji
wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba
ya majaribio 18. Aidha, kuendelea na
ujenzi wa kituo cha Bioscience katika
mkoa wa Morogoro; kuendelea na ujenzi
wa benki ya mbegu katika kituo cha TARI
Selian; kuendelea na ujenzi wa ofisi ya
Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma); na
kukamilisha ujenzi wa ofisi katika kituo
cha TARI Hombolo na ununuzi wa vifaa
vya Ofisi ya TARI Kihinga.

Mpendwa msomaji, katika Mwaka
wa fedha 2026/2027, TARI itaendelea
kutekeleza shughuli mbalimbali za utafiti
na ubunifu wa teknolojia za kilimo,
zikiwemo ugunduzi wa mbegu bora,
kanuni bora za kilimo, teknolojia za afya ya



DKT. THOMAS BWANA
MKURUGENZI MKUU - TARI

udongo, teknolojia za kudhibiti visumbufu
vya mazao (magonjwa na wadudu), tafiti
za uchumi jamii na masoko, pamoja na
utunzaji wa nasaba za mazao.

Mpango na Bajeti ya TARI katika mwaka
2026/2027 umeandaliwa kwa kuzingatia
Mpango Mkakati wa TARI (2025/2026–
2029/2030), mwongozo wa maandalizi ya
Mpango na Bajeti wa mwaka 2026/2027;
na masuala mtambuka ya Rushwa, VVU/
UKIMWI.

Vilevile, umezingatia miongozo ya Dira
(2050) pamoja Mpango Mkuu wa Sekta
ya Kilimo (Tanzania Agriculture Master
Plan).

Ili kupima kiwango cha mapokeo ya
teknolojia zilizohaulishwa kwa wadau,
TARI katika mwaka 2026/2027 imepanga
kufanya tathmini ya mapokeo (adoption)
kwa teknolojia 10 za kilimo.

Pia, ili kupima matokeo (impact) ya
matumizi ya teknolojia zilizohaulishwa,
TARI itafanya tathmini (6). Vilevile TARI
itafanya tathmini nyinginezo ikiwemo
masoko na masuala ya jinsia (3).
Mpendwa msomaji, TARI tuna mengi
ya kufanya ili kuleta tija kwa wakulima.
Nakusihi uendelee kuwa nasi katika
mfululizo wa matoleo ya Jarida la TARI
Habari ili uweze kufamamu mengi zaidi
kuhusiana na TARI pamoja na utekelezaji
wa majukumu yake katika kuimarisha
sekta ya kilimo nchini kupitia utafiti.



TARI YAIBUKA MSHINDI WA TATU MAONESHU YA SABASABA 2026

Dar es Salaam, Julai 2026

Tasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeibuka mshindi wa tatu katika mashindano ya mabanda bora yaliyoshirikisha taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakati wa Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba).

Ushindi huo umetokana na ubunifu wa banda la TARI, uwasilishaji wa teknolojia mbalimbali za kilimo, pamoja na namna taasisi hiyo ilivyoweza kutoa elimu na huduma kwa wadau wa sekta ya kilimo waliotembelea banda hilo.

Kupitia maonesho hayo, TARI imeendelea kutangaza matokeo ya tafiti zake ikiwemo teknolojia za mbegu bora, mbinu za kuongeza tija ya uzalishaji na suluhisho mbalimbali zinazolenga kuwasaidia wakulima nchini.

Uongozi wa TARI umeeleza kuwa ushindi huo ni chachu ya kuendelea kuboresha utoaji wa huduma na kuhakikisha matokeo ya tafiti yanafika kwa jamii ili kuchangia maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.





RAFIKI PLANTER YA LETA MAPINDUZI KILIMO, MAVUNO KUONGEZEKA HADI MAGUNIA 15 KWA EKARI

Na Lucy Ngowi

WAKULIMA nchini wanatarajiwa kuongeza uzalishaji na kupunguza gharama za upandaji wa mazao kufuatia maboresho ya zana ya kupandia mbegu ijulikanayo kama Rafiki Planter, iliyobuniwa na watafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Ukiriguru, Mwanza.

Akizungumza katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), mtafiti wa TARI Ukiriguru, Dawson Malela, amesema zana hiyo imeboreshwa kwa kuzingatia maoni ya wakulima ili iwe na ufanisi zaidi shambani.

Amesema mashine hiyo sasa ina injini yenye uwezo mkubwa, magurudumu ya matairi yenye upepo na inaweza kupanda ekari moja ndani ya dakika 45 hadi saa moja, tofauti na awali ambapo ilichukua zaidi ya saa moja.

Malela amesema zana hiyo hupanda mazao kama mahindi, pamba na alizeti kwa nafasi sahihi zinazoshauriwa kitaalamu, jambo

linaloongeza idadi ya mimea na mavuno.

“Wakulima wengi wamekuwa wakivuna magunia matano hadi sita kwa ekari kutokana na upandaji usiozingatia nafasi. Kwa kutumia Rafiki Planter wanaweza kuvuna magunia 12 hadi 15 kwa ekari,” amesema.

Ameongeza kuwa mashine hiyo huendeshwa na mtu mmoja, hutumia kiasi kidogo cha mafuta na inapunguza utegemezi wa vibarua wengi, hivyo kuokoa muda na gharama huku ikihakikisha mbegu zinapandwa kwa usahihi.

Amesema ubunifu huo umefanikishwa kwa ushirikiano wa TARI, COSTECH na Wizara ya Kilimo kupitia miradi ya maendeleo ya sekta ya kilimo.

Malela ameiomba Serikali kuendelea kuunga mkono uzalishaji wa mashine hiyo ili iwafikie wakulima wengi zaidi, akieleza kuwa teknolojia hiyo inaweza kuendeshwa na wanawake na vijana na hivyo kuchochea kilimo chenye tija na kuongeza ushiriki wa vijana katika sekta hiyo.





TARI YAPONGEZWA KWA KUWA MMOJA WA WASHINDI KATIKA KULINDA MAZINGIRA

Yaaahidi kuendelea kutoa elimu zaidi kuhusiana na kilimo hifadhi pamoja na kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazosaidia kutunza mazingira

77 Dar es Salaam

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imepongezwa kwa kupewa Cheti maalumu cha ushindi kwa kutambua mchango wake muhimu katika kulinda mazingira na kushiriki kwa ukubwa kwenye maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (SabaSaba) 2026.

Cheti hicho cha Ushindi kimetolewa tarehe 11/7/2026 na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu

wa Rais Muungano na Mazingira, Dkt Richard Muyungi katika kilele cha siku ya Mazingira kwenye maonesho yanayoendelea ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (SabaSaba).

Akiongea katika kilele cha Sherehe za Mazingira, Dkt. Muyungi amesema kila mtu ana jukumu la kulinda mazingira kwa sababu mazingira ni uhai na kuwataka wadau wote wa mazingira kuweka nia ya dhati ya kuendelea kuyalinda mazingira.

TARI katika maonesho hayo imetoa elimu na ushauri kuhusu kilimo pamoja na kugawa bure zaidi ya miche 50 ya matunda mbalimbali kwa wadau waliotembelea banda la TARI na kuhamasisha upandaji miti ya matunda ikiwa ni sehemu ya kuhimiza jamii kutunza mazingira.

Aidha, TARI imeendelea kutumia maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (SabaSaba) kusambaza teknolojia zake pamoja na matokeo ya utafiti kwa wadau.



XXXXXXXXXXXXXXXXXXXX



WAKULIMA na wananchi kwa ujumla wameshauriwa kupanda miti ya matunda, migomba na viungo viliyofanyiwa utafiti kwa kuwa yana faida kwa afya za walaji na kiuchumi.

Ushauri huo umetolewa na Mtafiti wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (TARI) Tengeru Tengeru Emmanuel Pallangyo wakati akizungumza na mwandishi wa Raia Mwema Digital.

Amesema TARI inafanya utafiti wa mazao mbalimbali kama miti ya matunda, viungo au vikolezo na mahindi, mpunga na mengine, hivyo wanashauri wakulima kupanda mazao hayo kwa kuwa yana faida nyingi.

Pallangyo amesema mazao kama ndizi, matunda na viungo au vikolezo yanaweza kulimwa kwenye bustani za nyumbani, hivyo wanawaomba wananchi kutembelea Banda la TARI lililopo kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), ili kujipatia mbegu bora zilizotafitiwa.

"Hapa sabasaba tuna

mbegu za mchaichai, parachichi, pera, migomba, korosho na nyingine nyingi, njooni mfaidi taasisi yenu," amesema.

Mtafiti huyo amesema mbegu zote ambazo wanazalisha zinangatia utafiti, ili kuwezesha wananchi wa maeneo yote ya Tanzania kutumia.

"Tunahamasisha matumizi ya viungo kwenye vyakula au chai kwa sababu tiba na chakula kuwa na harufu nzuri," amesema.

Pallangyo amesema pamoja na TARI kuzalisha mbegu nyingi kitafiti, bado wakulima wanaamini kwenye mbegu zilizopitwa na wakati, hivyo kukosa tija kwenye uzalishaji.

Mkulima wa zao migomba kutoka Chalenzi wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, Martin Mayengela amesema umevutiwa na mazao ya yanayozaliswa TARI na ndio maana amenunua na kwenda kupanda.

"Mimi nimekuja hapa kununua miche ya migomba na parachichi nikapande shambani kwangu naamini itaenda kufanya vizuri," amesema.



MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO ATEMBELEA BANDA LA TARI SABASABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Bi. Siwema Hamoud Jumaa, ametembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea

katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere.

Akiwa katika banda hilo, Bi. Jumaa alipata maelezo kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na TARI, ikiwemo utafiti wa kilimo, uzalishaji wa mbegu bora, teknolojia za kuongeza tija ya mazao, pamoja na utoaji wa mafunzo na ushauri wa

kitaalamu kwa wakulima na wadau wa sekta ya kilimo.

Ziara hiyo imeonesha umuhimu wa ushirikiano kati ya TARI na mamlaka za serikali za mitaa katika kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kilimo zinazochochea ongezeko la uzalishaji na maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.





PROF. MSOFFE AITAKA TARI KUONGEZA JUHUDI ZAIDI JUU YA UTAFITI WA ZANA ZA KILIMO

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo anayeshughulikia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula Prof. Peter Msoffe ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kuongeza juhudi katika utafiti na ubunifu wa zana za kilimo zilizo rafiki na rahisi kutumiwa na mkulima.

Prof. Msoffe ametoa agizo hilo alipotembelea banda la TARI katika Viwanja vya Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba). Pia, alipongeza jitihada zinazofanywa na TARI katika utafiti wa udongo, mbegu, visumbufu vya mimea

pamoja na uongezaji thamani wa mazao mbalimbali baada ya mavuno na kueleza kuwa TARI imejijengea sifa kubwa katika uzalishaji wa mbegu bora kwa mfano mpunga aina ya SARO 5 (TXD 306) ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji na tija kwa mkulima.

Akiwa katika banda la TARI, Prof. Msoffe alibainisha kuwa, kwa sasa TARI inajulikana zaidi kwa matokeo ya utafiti wa mbegu bora na afya ya udongo lakini kwa upande wa zana za kilimo bado jitihada zaidi zinatakiwa ziongezwe katika kasi ya ubunifu wa zana bora za kilimo, rahisi na

rafiki kwa mkulima ili kumpunguzia mzigo mlengwa katika shughuli za kilimo ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji na kuchochea kilimo endelevu, chenye tija na kinachochangia maendeleo ya sekta ya kilimo na Taifa kwa ujumla.

Wadau na wananchi mbalimbali wameendelea kutembelea banda la TARI na kupata elimu ya teknolojia za Kilimo katika mnyororo wa thamani ikiwa ni Pamoja na teknolojia baada ya mavuno. Pia, wamepata fursa ya kununua miche ya mazao mbalimbali ya migomba, matunda, mboga, viungo na vikolezo.



TEKNOLOJIA ZA TARI ZANG'ARA KATIKA UHIFADHI WA MAZINGIRA SABASABA



Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeendelea kuonesha dhamira yake ya kulinda mazingira kupitia ubunifu wa teknolojia mbalimbali rafiki kwa mazingira zinazolenga kuongeza tija katika sekta ya kilimo huku zikihakikisha usalama wa watumiaji na uhifadhi wa mazingira.

Miongoni mwa teknolojia hizo ni uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali pamoja na teknolojia za uongezaji thamani wa mazao baada ya mavuno, ambazo zimewasilishwa katika Green Revolution Challenge inayoendelea sambamba na Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba). Shindano hilo linaangazia mchango wa taasisi na wadau mbalimbali katika uhifadhi wa mazingira kupitia ubunifu na matumizi ya teknolojia endelevu.

Katika kutembelea banda la TARI, muongozaji wa Green Revolution Challenge, Mr. Tree, alipata fursa ya kujifunza kuhusu teknolojia mbalimbali zinazobuniwa na taasisi hiyo kwa ajili ya kukuza kilimo endelevu na hifadhi ya mazingira.

Miongoni mwa ubunifu zilizovutia zaidi ni teknolojia ya utengenezaji wa mkaa mbadala unaotokana na mabaki ya zao la mchikichi, teknolojia inayochangia kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti na hivyo kusaidia kuhifadhi misitu na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kupitia ubunifu huo, TARI inaendelea kuthibitisha nafasi yake katika kuendeleza teknolojia za kilimo zinazochochea uzalishaji wenye tija, zinazoendana na uhifadhi wa mazingira na kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa.

TARI katika kipindi cha maonesho ya 77 iligawa bure zaidi ya miti 50 ya matunda mbalimbali ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuunga mkono Serikali katika suala zima la kuhamasisha jamii kutunza mazingira.





TARI YAENDELEA KUELIMISHA WADAU KUHUSU TEKNOLOJIA ZA KILIMO

TARI Yaendelea Kuelimisha Wadau kuhusu Teknolojia za Kilimo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya SabaSaba

Wadau mbalimbali wanaotembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) wanaendelea kupatiwa elimu kuhusu teknolojia mbalimbali za kilimo katika mnyororo mzima wa

thamani wakati wa Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (SabaSaba), yanayofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Maonesho hayo yanaongozwa na kaulimbiu isemayo: "Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya SabaSaba: Fahari ya Tanzania."

Kupitia ushiriki wake katika

maonesho hayo, TARI inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kanuni bora za kilimo, matumizi ya teknolojia za kisasa katika uzalishaji, pamoja na mbinu za uongezaji thamani wa mazao mbalimbali ya kilimo. Lengo la elimu hiyo ni kuongeza tija, kuimarisha uzalishaji wenye ushindani, na kuchochea maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.





XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX

Kamishna wa Huduma za Urekebu wa Jeshi la Magezea, CP Amina Kavirondo, ametembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea katika Viwanja vya Mwl. JK Nyerere, na kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa na TARI kwa wadau wa sekta ya kilimo.

Akizungumza alipotembelea Banda hilo Kamishna Kavirondo ameipongeza TARI kwa kazi kubwa

na mchango wake katika kufanya utafiti wenye tija katika sekta ya kilimo.

Aidha Kamishna Kavirondo ametoa wito kwa TARI kushirikiana na Jeshi la Magezea Tanzania kuwapatia wafungwa mafunzo ya uongezaji thamani wa mazao mbalimbali yanayofanyiwa utafiti na taasisi hiyo huku akisisitiza kuwa kuwaweka wafungwa kama moja ya makundi maalumu kama ilivyo kwa makundi mengine.

Amesema ushirikiano huo utawajengea wafungwa ujuzi wa vitendo utakaowawezesha kujiajiri

na kujipatia kipato halali baada ya kumaliza vifungo vyao, hivyo kupunguza uwezekano wa kurejea katika vitendo vya uhalifu.

"Tukiwapa maarifa na stadi za kuongeza thamani ya mazao, tunawapa fursa ya kuanza maisha mapya yenye tija na kuwa sehemu ya maendeleo ya taifa," amesema CP Kavirondo

TARI imeendelea kuthibitisha dhamira yake ya kuendeleza tafiti na ubunifu unaochochea maendeleo ya kilimo, usalama wa chakula na uongezaji thamani wa mazao yanayofanyiwa utafiti.





MKUU WA WILAYA YA KILWA ATEMBELEA BANDA LA TARI SABASABA

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Mhe. Mohamed Nyundo, ametembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba, jijini Dar es Salaam, ambapo alipata fursa ya kufahamu zaidi

huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Akiwa katika banda hilo, Mhe. Nyundo alipokea maelezo kutoka kwa watafiti wa TARI kuhusu teknolojia mbalimbali za kilimo, mbegu bora za mazao pamoja na namna taasisi hiyo inavyoweza wakulima kupata matokeo bora kupitia

tafiti na ubunifu wa kilimo.

Mkuu huyo wa Wilaya alieleza kuridhishwa na maonesho ya TARI, akipongeza juhudi za taasisi hiyo katika kuleta teknolojia na maarifa ya kilimo yanayolenga kuongeza tija kwa wakulima na kuchangia maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.





KAIMU MKURUGENZI MKUU WA COASCO AIPONGEZA TARI KWA UZALISHAJI WA MBEGU BORA

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Tanzania (COASCO), CPA Jeremiah Mugeta, ameipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa juhudi zake za kuzalisha mbegu bora zenye tija ambazo zimeendelea kuwanufaisha wadau wa sekta ya kilimo nchini.

CPA Mugeta alitoa pongezi hizo

alipotembelea banda la TARI katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), ambapo alipata fursa ya kujionea teknolojia mbalimbali za kilimo na mbegu bora zilizofanyiwa utafiti.

Akizungumza baada ya kutembelea banda hilo, amewahimiza wakulima nchini kutumia mbegu bora zilizofanyiwa

utafiti ili kuongeza tija, kukabiliana na changamoto za uzalishaji na kuboresha kipato chao.

Aidha, amesema vyama vya ushirika vimeendelea kunufaika na matokeo ya tafiti zinazofanywa na TARI, akieleza kuwa uzalishaji kupitia vyama hivyo umeongezeka kutokana na upatikanaji wa mbegu bora na zilizoboreshwa zinazozalishwa na TARI.





TARI YAENDELEA KUONESHA TEKNOLOJIA ZA KILIMO KATIKA MAONESHU YA SABASABA

Dar es Salaam, Julai 10, 2026

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeendelea kupokea wageni mbalimbali katika banda lake wakati wa Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), ambapo viongozi kutoka taasisi mbalimbali wamepata fursa ya kujifunza kuhusu tafiti, teknolojia na huduma zinazotolewa na taasisi hiyo kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Miongoni mwa viongozi waliotembelea banda la TARI ni

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania, Prof. Kenneth Bengesi, pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania, Bw. Francis Alfred.

Katika ziara hiyo, viongozi hao walipokea maelezo kutoka kwa wataalamu wa TARI kuhusu tafiti mbalimbali zinazofanywa na taasisi hiyo, hususan maendeleo ya mbegu bora za mazao, teknolojia za kuongeza tija kwa wakulima pamoja na namna TARI inavyohamisha matokeo ya tafiti kwenda kwa jamii.

Viongozi hao walieleza kuridhishwa na mchango wa TARI

katika kuendeleza kilimo nchini kupitia ubunifu wa kisayansi na teknolojia zinazolenga kuongeza uzalishaji na kuboresha maisha ya wakulima. Aidha, walisitiza umuhimu wa kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za umma ili kuhakikisha matokeo ya tafiti yanafika kwa walengwa na kuchangia ukuaji wa sekta ya kilimo na uchumi wa taifa.

Maonesho ya Sabasaba yamekuwa jukwaa muhimu kwa TARI kuonesha mchango wake katika utafiti wa kilimo, uendelezaji wa teknolojia na utoaji wa elimu kwa wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo.



RUHUKA: MDUDU ANAYETISHIA ZAO LA KAHAWA, TARI YAJA NA SULUHISHO

Na Mwandishi Wetu

KAHAWA ni miongoni mwa mazao ya biashara yanayochangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa Tanzania kupitia mauzo ya nje na kipato cha wakulima.

Hata hivyo, mafanikio ya zao hilo yanaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, mojawapo ikiwa ni mashambulizi ya wadudu waharibifu.

Miongoni mwa wadudu hao, ruhuka ametajwa kuwa adui mkubwa wa zao la kahawa duniani.

Kwa mujibu wa Mtafiti Mwandamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha TaCRI Lyamungu, Dkt. Godstevens Maro, ruhuka ni mdudu anayeshambulia punje za kahawa kwa kutoboa matunda na kuingia ndani ya punje.

Kitendo hicho huharibu ubora wa kahawa na kupunguza thamani yake sokoni, hivyo kuwaingizia wakulima hasara kubwa.

Dkt. Maro anazungumza hayo katika Maonesho ya 50 ya Sabasaba yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Anasema mdudu huyo si tatizo la Tanzania pekee, bali ni changamoto inayowakabili wazalishaji wa kahawa duniani.

Nchi kama Colombia zimekuwa zikiwekeza katika tafiti za kudhibiti ruhuka kwa kutumia mitego maalumu ya kumvutia na kumtega.

Kutokana na uzoefu huo, watafiti wa TaCRI wameboresha teknolojia hiyo ili iendane na mazingira ya Tanzania.

Mtego huo umetengenezwa kwa kutumia vifaa vinavyopatikana kwa urahisi, huku ukitumia vimiminika kama spiriti au pombe za kienyeji kuvutia wadudu hao.

Kwa mujibu wa watafiti, mtego mmoja unaweza kunasa hadi wadudu ruhuka 600 kwa kipindi cha wiki moja.

Hii inaonyesha kuwa teknolojia hiyo inaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa idadi ya wadudu wanaoshambulia mashamba ya kahawa ikiwa wakulima wataitumia kwa usahihi.

Faida nyingine ya mtego huo ni kwamba ni wa gharama nafuu na unaweza kutengenezwa na mkulima mwenyewe bila kuhitaji vifaa vya gharama kubwa.

Hali hiyo inaufanya kuwa suluhisho linalofaa kwa wakulima wadogo na wakubwa.

Kwa sasa, ruhuka ameendelea kuongezeka katika mashamba ya kahawa aina ya Arabica na Robusta nchini Tanzania.

Wataalamu wanaonya kuwa bila kuchukua hatua za haraka, mdudu huyo anaweza kuendelea kupunguza uzalishaji na ubora wa kahawa ya Tanzania.

Dalili za mashambulizi ya ruhuka ni pamoja na kuwepo kwa tundu moja au zaidi kwenye kitovu cha tunda la kahawa, iwe tunda bado ni bichi au limeiva.

Wakulima wanashauriwa kukagua mashamba yao mara kwa mara ili kubaini dalili hizo mapema na kuanza kutumia mbinu za udhibiti kabla uharibifu haujaongezeka.

Mbali na matumizi ya mitego, wataalamu wanasisitiza umuhimu

wa kutumia mbinu za udhibiti husishi wa wadudu, ikiwa ni pamoja na usafi wa shamba, kuvuna kwa wakati, kuondoa matunda yaliyoshambuliwa na kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo.

Kadiri sekta ya kahawa inavyoendelea kuwa nguzo muhimu ya uchumi wa Tanzania, matumizi ya teknolojia rahisi na bunifu kama huu wa TaCRI yanaweza kuwa suluhisho muhimu katika kupunguza hasara zinazotokana na wadudu waharibifu na kuongeza uzalishaji wa kahawa yenye ubora unaokidhi mahitaji ya soko la dunia.



Mdudu ruhuka (Coffee Berry Borer) ni mdudu hatari anayeshambulia zao la kahawa kwa kutoboa matunda na kula punje zake